
MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu




# Umahuluti wa Kiisimu Katika Nyiso za Wabukusu

Eric Wamalwa*

*Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma, Kenya*

**IKISIRI**

Makala hii inapambanua udhihirikaji wa umahuluti wa kiisimu katika nyiso za Wabukusu zinazotokana na tohara ya Wabukusu kwa mtazamo kuwa tamaduni zinapotagusana zinaathiriana. Tamaduni zenye nguvu hupata nafasi ya kuathiri tamaduni nyingine. Tohara ni mivigha maarufu ambayo ni utambulisho wa jamii ya Wabukusu. Licha ya mabadiliko yanayoathiri jamii katika majira haya ya utandawazi, tohara ya Wabukusu ni mojawapo ya tamaduni ambazo zimedumishwa na kuhifadhiwa. Utafiti ulichunguza nyiso na miviga ya tohara ili kubaini utamaduni wenye nguvu ulioegemezwa katika nyiso za Wabukusu pamoja na kupambanua jinsi miundo ya kiisimu inadhihirisha umahuluti katika nyiso hizo. Makala hii imeongozwa na nadharia ya Umahuluti wa Kiutamaduni. Data ilikusanywa kwa mbinu ya usikilizaji wa kanda za nyiso za Kibukusu na uchanganuzi wa yaliyomo. Data ilichanganuliwa kithamano na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yameonesha kwamba umahuluti wa kiisimu katika nyiso za Wabukusu unajitokeza kupitia miundo mbalimbali ya kiisimu kama vile ujumuilugha, ukopaji kupitia utohozi, miundo ya kisintaksia kama vile kuchanganya na kubadili msimbo na tafsiri.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Umahuluti,
Utamaduni,
Nyiso,
Wabukusu

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 23 Juni 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 1 Julai 2025
Tarehe ya Kukubalika: 10 Julai 2025
Mtandaoni: 29 Agosti 2025

## 1. Utangulizi

Tohara ya Wabukusu ina misingi yake katika kisasili cha jagina aliyeitwa Mango. Asemavyo Simiyu (2015), tohara hii ni utamaduni ambao umedumishwa tangu kufufuliwa na Mango mwaka wa 1800 katika tukio la historia la kuuwa joka yabebe. Kwa mujibu wa kisasili hiki, joka hili liliwala watu na wanyama na kusababisha maafa mengi kiasi cha kuwaogofya wenyeji. Katika msako wa kuliua, lilimla mwana wa Mango na hapo akaapa kulisaka na kuliua. Siku hiyo alikuwa amejificha kwenye umio wa pango karibu na gogo. Magharibi ilipowadia, joka hilo lilirejea huku Mango akiwa amelisubiri kwa upanga. Lilikagua mazingira na lilipokuwa linaingia, alilikata kichwa. Tukio hilo liliwafurahisha wanajamii walioamua kumtawaza kama shujaa wa vita kwa kumpasha tohara. Alipopelekwa kupashwa tohara mamake alilia kwa hofu na inasemekana kuwa maneno aliyotamka yalishirikishwa kwa wimbo maarufu wa sioyayo. Tangu enzi hizo wimbo huo huimbwa kila asubuhi wavulana wanapopelekwa mtoni (syetosi) kupakwa tope kabla ya kuelekea nyumbani ili kutahiriwa. Mwaka huo vijana wote waliokuwa na umri sawa na Mango walisakwa na kupashwa tohara. Tangu hapo basi, kukawa na itikadi ya tohara katika umri au vikundi vya marika (bibingilo). Tohara hii huwa kwa mzunguko wa mdwara na huratibiwa kwa kuzingatia muda na matukio muhimu katika jamii.

Tohara katika jamii nyingi ni daraja la kutoka utotoni kuingia utu uzima. Asemavyo Simiyu (2011), jamii ya Wabukusu huendeleza mivigha ya tohara ya wanaume na haithamini mwanamume asiyetahiriwa, (siembekho). Ni itikadi ya jamii hii kuwa lazima kila mvulana atahiriwe. Kila mwanamume ana deni la kupashwa tohara. Mwanamume akifa kabla ya tohara, lazima atimize mivigha hii ndipo azikwe na tohara hiyo hufanywa kwa gharama kubwa. Kwa kuzingatia utekelezaji katika muktadha wa kisasa wa mfumuko wa utamaduni, tohara hii hutimizwa kuwili; kuna wale waendao hospitalini na wanaotahiriwa kiutamaduni nyumbani. Katika tohara za nyumbani, ngariba (omukhebi) humtahiri mvulana katika sehemu teule (khuluyia). Kabla ya siku ya tohara, watahiriwa hutembea kwa maboma ya jamaa, jirani na marafiki wakipiga kengele (chinyimba) na kuimba nyiso-khulanga. Lengo huwa kuwajulisha uamuzi wao wa kupashwa tohara na kuwaalika ili washiriki na kushuhudia tikio hilo siku ya tohara.

Nyimbo miongoni mwa Wabukusu ni tukio la kijamii. Wanajamii wanapojumuika katika harusi, mazishi na unywaji pombe, nyimbo hushirikishwa kwa ajili ya burudani, kufahamishana maarifa, na kudumisha umoja na ushirikiano. Kwa hiyo wimbo uimbwao hutegemea tukio husika la kijamii na ala za muziki huweza kuhusishwa. Mojawapo wa nyimbo maarufu katika jamii

* Mwandishi Mkuu. Simu: +254724609705; Barua Pepe: ewalela@kibu.ac.ke
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Eric W. (2024). Umahuluti wa Kiisimu Katika Nyiso za Wabukusu. Jarida la Kiswahili Sanifu, 2(1), 30 – 39.

© 2025 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

ya Wabukusu ni nyiso ambazo huongozwa na waimbaji wenye tajriba.

Wamitila (2004) anasema kuwa nyiso ni nyimbo zinazohusishwa na jando na unyago, na kwamba, huimbwa na jamii ambazo huwa na sherehe za tohara. Aidha, Matei (2011:99) anafafanua nyiso kuwa "ni nyimbo ambazo huimbwa katika shughuli za jando." Fasili pana zaidi ya nyiso imetolewa na Habwe & Zaja (2019) wanaosema kwamba, "nyiso hurejelea nyimbo zinazoimbwa katika sherehe, mifanyiko, matambiko, na maandalizi ya jando". Kwa mujibu wa maelezo haya, nyiso zinaweza kuimbwa wakati wa sherehe, katika mchakato wa maandalizi ya sherehe, wakati wa matambiko ndani ya sherehe, ilmuradi tukio husika linahusu tohara. Katika jamii ya Wabukusu, nyiso huimbwa tangia kipindi cha kijana kuanza maandalizi hadi anapokuwa akitoka jandoni, baada ya kupona. Baadhi ya jamii zinaimba nyimbo hizi usiku wa kuamkia siku ya kupasha tohara ilhali wengine huimba kuambatana na matambiko mbalimbali yanayozunguka mivigha ya tohara. Maudhui yanayojitokeza katika nyiso huwa ya kufundisha maadili kama vile staha na usafi, heshima, mahusiano mema, umuhimu wa uaminifu na haja ya kuheshimu utamaduni (Habwe & Zaja, 2019). Hata hivyo, maudhui hayo hutofautiana kutoka kwa nyiso za jamii moja hadi nyingine. Jambo hili linazua haja ya uchunguzi kufanywa ili kupambanua miundo, majukumu na maudhui mbalimbali katika jamii husika. Aidha, tafiti zilizofanywa awali zinadhihirisha kuwa jamii inakumbwa na mabadiliko katika miundo ya kisiasa, kidini, kiuchumi na usasa ambayo, yamesababisha mabadiliko katika nyimbo ili kukabiliana na mitindo ya kiutamaduni (Wanyama, 2005). Jambo hili linazua haja ya uchunguzi kufanywa ili kuyaangazia mabadiliko hayo. Ni katika muktadha huu ndipo nyiso za Wabukusu zimechanganuliwa kwa lengo la kupambanua kudhihirika kwa miundo ya kiisimu katika muktadha wa umahuluti.

## 2. Umahuluti wa Kiisimu

Umahuluti, kwa mujibu wa Habwe & Zaja (2019), ni dhana inayotumika katika nadharia za baada-ukoloni kurejelea michakato ya uibukaji wa mifumo changamani ya kiutamaduni na kijamii ambapo tamaduni tofauti huingiliana. Ni uzazi mtambuko wa utamaduni. Umahuluti ni uhusishaji jumuifu wa vipengele vya tamaduni mbalimbali. Umahuluti wa kiutamaduni hauna nia ya kuzua ukinzani au mtafaruku baina ya tamaduni bali ni njia ya kuwezesha elimu au maarifa mengine ambayo hayakuwepo kuingizwa katika utamaduni lengwa kwa minajili ya kuufanya kuwa thabiti. Umahuluti hujaribu kuondoa mipaka na kuimarisha upya tamaduni kati ya watu, jamii, nakabila na nchi. Kwa hiyo, umahuluti si tukio la siku moja bali tendo linaloendelea kadri jamii na tamaduni zinavyoendelea kutagusana (Demska, 2019).

Bhabha (1997) anaeleza kuwa, lugha zote zina sifa ya umahuluti. Anasema kwamba tamaduni zinapotagusana, zinaathiriana ambapo utamaduni wenye nguvu au wenye athari kubwa hupata nafasi ya kuathiri utamaduni mwingine, jambo linalojidhihirisha kupitia kwa lugha ya watu. Lugha ni chombo cha kueleza tunu tofauti zilizofungamana na maumbile ya kimila, fikira, maarifa, imani, adabu na utamaduni wa jamii kwa ujumla. Shatry (1996) anaeleza kuwa lugha inasadifu msingi wa kukuza, kuendeleza na hata kubuni uzushi mpya katika mirathi ya utamaduni, mila na hulka za kijamii ambapo neno jipya huwa msingi wa wazo jipya.

Dhana ya umahuluti wa kiisimu imefasiliwa na wataalamu wengi (Bakhtin, 1981; Bhabha, 1994; Manessy, 1995). Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), umahuluti wa kiisimu ni mchanganyiko wa fahamu za lugha ndani ya kauli moja, unaowezesha uhakiki wa itikadi za kijamii. Hivyo, mandhari ya lugha inaweza kuchukuliwa kuwa na umahuluti wakati lugha nyingi na nyaraka nyingi zinafanya kazi ndani yake kwa wakati mmoja. Naye Bhabha (1994), anaeleza kwamba umahuluti wa kiisimu ni ukiukaji wa mifumo ya utawala wa kikoloni, ambapo jamii zilizotawaliwa na wakoloni huunda upya lugha wazizolazimishiwa za kikoloni ili kuumba fursa za mawasiliano ya kitamaduni na mapatano ya kiisimu. Naye Manessy (1995) anaangazia umahuluti katika muktadha mpana wa Kiafrika anaposema kuwa ni ubunifu wa unaoakisi urekebishaji wa utambulisho, baada ya ukoloni. Kutokana na fasili hizi, tunahitimisha kuwa umahuluti wa kiisimu unarejelea mchanganyiko wa vipengele kutoka kwa lugha nyingi au lahaja ndani ya mfumo mmoja wa kimawasiliano, na hivyo kusababisha mazoea mapya ya kiisimu.

Fasili zilizorejelewa zimedhihirisha mambo yafuatayo kuhusu umahuliti wa kiisimu: Mosi, hutokea katika mahusiano baina ya lugha za kikoloni na lugha asilia za kiafrika. Pili, umahuluti wa kiisimu ni ubunifu wa kimawasiliano. Tatu, unahusisha uingizwaji wa vipengele vya lugha kutoka lugha nyingine kuingia lugha pokezi. Nne, umahuluti wa kiisimu huenda sambamba na utamaduni wa jamii kwani lugha ni kipengele mojawapo muhimu katika utamaduni wa jamii. Hatimaye, umahuluti wa kiisimu unajitokeza kutokana na mawasiliano ya lugha, mara nyingi katika miktadha ya baada-ukoloni, uhamiaji, biashara, au ukuaji wa miji na maendeleo ya kiteknolojia. Tunakubaliana na Demska (2019) anaposema kwamba kama kipengele cha umahuluti wa kitamaduni, umahuluti wa kiisimu unahusiana kwa karibu na mazoea ya kila siku yanayohusukazi, chakula, nguo, usafi, afya, tafrija, sherehe, mawasiliano na kadhalika.

Tohara ni mivigha maarufu ambayo ni utambulisho wa jamii ya Wabukusu. Licha ya mabadiliko yanayoathiri jamii katika majira haya ya utandawazi, tohara ya Wabukusu ni mojawapo ya tamaduni zilizodumishwa na kuhifadhiwa. Miviga hii huambatana na nyimbo, ambapo kila sehemu ya matambiko na mivigha inazihusisha. Maudhui katika nyiso yanajumuisha matambiko na desturi za jamii husika. Suala linalozuka ni udhihirisho wa jinsi uhifadhi wa utamaduni wa tohara unavyotagusana na mtazamo mpya wa jamii wa kujitambulisha katika ulimwengu wa utandawazi. Lengo kuu la makala hii lilikuwa kupambanua umahuluti wa kiisimu unavyodhihirika katika nyiso na miviga ya tohara za Wabukusu. Katika kulitekeleza, tulidhamiria

kubainisha utamaduni wenye nguvu ulioegemezwa katika nyiso za Wabukusu na kuainisha maumbo ya udhihirikaji wa umahuluti katika nyiso za Wabukusu.

## 2.1. Uhakiki wa Maandishi

Nyiso za Wabukusu ni eneo ambalo limevutia uchunguzi wa wataalamu wengi. Mathalan, Wanyama (2005) alichunguza muundo na yaliyomo katika nyiso za Wabukusu. Msukumo wa utafiti huo ulitokana na mabadiliko ya kiteknolojia, ujenzi wa miji, viwanda, kuzuka kwa gonjwa sugu la UKIMWI ambalo limesababisha mabadiliko makubwa katika jamii. Alieleza kuwa mabadiliko katika jamii yameathiri muundo, yaliyomo, majukumu na utendaji wa nyimbo katika sherehe. Utafiti huo ulipambanua miundo mbalimbali, maana na majukumu ya nyimbo hizo katika muktadha wa utawala wa kibepari, na mwingiliano wa dini ambao ni tofauti na utamaduni wa jamii. Alibaini kuwa nyiso za Wabukusu zilizama katika visasili, miiko na itikadi mbalimbali. Aidha zilijikita katika muktadha fulani. Utafiti huo ulipambanua kuwa mabadiliko katika siasa, uchumi na jamii yaliathiri mwelekeo, majukumu na utendaji wa nyiso. Aidha alieleza kuwa mabadiliko ya muundo na mpangilio na viambatanishi viliathiriwa na dini, teknolojia na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Dhima ya nyiso za Wabukusu ni eneo lingine lililochunguzwa. Simiyu (2011) alilenga kutambua umuhimu wa nyiso za Wabukusu katika mabadiliko yaliyopo katika jamii. Mabadiliko hayo yalihusisha yale ya kiteknolojia, ukuaji na upanuzi wa miji na viwanda ambayo yalisababisha mfumuko wa tabia na jinsi ya maisha ya watu. Alifafanua kuwa mambo haya yalizua changamoto katika jamii. Akadai kwamba, kutokana na mababiliko hayo, kumetokea tungo mpya zenye mada mpya na mitindo mipya ili kutimiza matakwa ya mitindo iliyozuka ya utamaduni endelevu. Isitoshe, uchunguzi huo ulitambua kuwa nyimbo za tohara zilitekeleza dhima ya kukemea maovu na kudumisha maadili. Alipambanua kuwa muundo na maudhui katika nyiso za Wabukusu yamebadilika ili kuhusisha masuala ibuka kwa lengo la kufahamisha na kuelimisha.

Utafiti mwingine kuhusu suala la tohara na nyiso ulifanywa na Simiyu (2015). Utafiti wake ulihusu mwingilianotanzu katika utendaji wa mivigha ya embalu na mwaka kogwa. Kitovu cha utafiti huo kilitokana na haja ya kupigania nafasi stahiki ya lugha na fasihi ya Mwafrika na hali ya tafiti za awali zilizohusu uchambuzi wa utanzu mojamoja. Utafiti huo ulilenga kuthibitisha kuwa, miviga ya embalu na mwaka kogwa ilijengwa na kuamilishwa kupitia mwingilianotanzu kwa msaada wa fanani, hadhira, muktadha na vivigha maalum. Utafiti huo ulibainisha kuwa, miviga ya embalu na mwaka kogwa iliumbwa na kuamilishwa kutokana na uchanganyikaji wa tanzu zinazoingiliana kikorasi na kimatini, kutenguana, kujinyambua na kusemezana wakati wa utendaji; nyiso zikiwa mojawapo wa vipengele muhimu katika uchambuzi. Matokeo ya utafiti huo yalithibitisha kuwa fasihi simulizi ya Kiafrika ni mfumo timilifu wa maarifa ambao unajengwa kwa tanzu na vipera visivyoweza kutenganishwa katika hali halisi ya utendaji. Utafiti huo ulipambanua mwingiliano wa tanzu kwa kurejelea muundo wake ila huu unachunguza mwingiliano wa utamaduni lugha kama unavyodhihirika katika nyiso.

Simiyu & Mukhwana (2016) wamechunguza leksia zinazotumiwa katika nyiso za Wabukusu kurejelea wanaume na wanawake. Lengo likiwa kutambua jinsi leksia hizi huwasawiri wanaume na wanawake na kubainisha jinsia zilikoegemea sana. Utafiti huo ulibaini kuwa leksia zilizotumiwa hufasiri maana inayodokezwa katika kamusi. Aidha matokeo yalionesha kuwa ilikuwa vigumu kubaini upande ulioegemewa kati ya jinsia ya kiume na kike kwani msamiati uliotumiwa ulitegemea kusudi la wimbo ulioteuliwa. Utafiti huo sawia na huu umechambua utanzu wa nyiso lakini tofauti iliyopo ni kuwa utafiti huu ulilenga kufafanua jinsi nyiso zimedhihirisha umahuluti wa kiisimu kutokana na mtagusano wa tamaduni mbalimbali.

Tafiti kuhusu nyiso zinaendelea kufanywa, mbali utafiti wa awali. Tafiti hizo ama zinahusu muundo wa nyiso, majukumu yake katika ulimwengu wa utandawazi, maudhui husika na jinsi zinavyozungumzia suala la jinsia au mwingiliano wake na tanzu nyingine za fasihi simulizi. Mathalan, Koech (2024) ameshugulikia suala la umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi miongoni mwa Wanandi. Uchunguzi huo ulilenga kubainisha umahuluti wa utamaduni katika nyimbo teule za harusi kwenye kipindi cha Tumdo katika runinga ya Kass. Alichunguza vipengele vya utamaduni wa jadi katika nyimbo na akaelezea mabadiliko ambayo yamefanywa na wasanii kwenye vipengele vya jadi. Alihitimisha kuwa nyimbo za harusi haziwezi kuchunguzwa bila kuhusishwa na mivigha ya harusi. Ni bayana kwamba tafiti nyingi nchini zimejikita katika uchunguzi wa umahuluti katika mwelekeo wa kifasihi, Makala hii imechangia maarifa kuhusu umahuluti kwa kupambanua suala la umahuluti wa kiisimu na miundo inayoudhihirisha mintarafu ya mtagusano ya utamaduni wa jamii ya Wabukusu na tamaduni nyingine kupitia nyiso za Wabukusu.

## 2.2. Misingi ya Kinadharia

Uchambuzi Dhana ya umahuluti imechochea utafiti katika taaluma nyingi. Anavyoeleza Ackermann (2012) dhana hii iliibuliwa katika karne ya ishirini ambapo ilitumiwa sana katika mtazamo wa kijamii kwa tafiti za Robert Young na wengine. Kati ya miaka 1980 na 1995, tafiti hizi zilihama kutoka mtazamo wa kihistoria nao watafiti wakaelekeza uchunguzi katika uwanja wa Biolojia. Baada ya hapo dhana hii ilipata mtazamo wa kianthropolojia katika tafiti za Robert Ezra Park, Alejo Carpentier na wengine baina ya miaka ya 1864-1994. Utafiti kuhusu umahuluti ulipokea mtazamo mpya katika utafiti wa Levi- Strauss katika miaka 1908-2009. Alifanya uchunguzi kuhusu umahuluti kwa kurejelea visasili. Alitaja kuwa visasili vilidhihirisha uwili pale ambapo vilishirikisha vitu vya kiasili au kimsingi katika utamaduni wa jamii na kuundwa upya ili kutosheleza muktadha husika; dhana aliyoiita bricolage. Katika miaka ya 1960, nadharia ya umahuluti ilichunguzwa kwa mtazamo wa kianthropolojia na kiisimu. Mathalani Homi Bhabha (1997) na mwanaisimu Bakhtin (1981) walichunguza muundo katika utamaduni wa jamii ambapo walitambua

kuwepo kwa utamaduni wenye nguvu unaoegemezwa katika tamaduni mbalimbali katika mitagusano ya jamii. Utafiti huu utazingatia mtazamo huu wa Bakhtin (1981) katika mwendelezo wake wa nadharia hii.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981), umahuluti unashirikisha jinsi lugha yoyote inaweza kudhihirisha sauti mbili tofauti ambapo sauti moja inavumbua na kuvumisha nyingine katika kauli moja. Anaitazama lugha katika muktadha wa lugha moja kuangaza nyingine. Hivyo basi, Bakhtin anatazama lugha kuwili; matumizi ya zaidi ya lugha moja katika matini moja na pia sauti mbalimbali katika maandishi ya riwaya kwa madhumuni ya tamaduni hizi kukaa pamoja bila kukwaruzana. Mtazamo huu ulisukumwa na wazo kuwa kila uchao, lugha hutagusana kwa lengo la kudhihirisha mtazamo mpya wa kilimwengu. Katika kufanya hivyo, mchanganyiko huu wa lugha unaweza kuwa wa kimakusudi (umahuluti wa kimakusudi) au usio wa makusudi (umahuluti usio wa kimakusudi).

Umahuluti wa kimakusudi unahusu kuweka kwa vipashio tofauti kimakusudi. Hii inahusisha: ukopaji-utamaduni mmoja unakopa kutoka kwa utamaduni mwingine katika hali ya makubaliano fulani. Kuna pia kuchanganya leksia za lugha mbili tofauti ili kuunda leksia moja inayohusisha asili mbili. Pia kuna tafsiri ya utamaduni mpya wa lugha kwa lugha nyingine ambapo msamiati, virai au vishazi kutoka kwa lugha moja huingizwa kwa lugha nyingine. Kuna pia umahuluti usio wa makusudi ambao ni tukio la kila siku la kuchanganya lugha.

Tumeitumia nadharia hii katika utafiti huu kutambua utamaduni pendwa ulioegemezwa kwenye nyiso, maudhui husika na jinsi uhulutishaji wa kiisimu ulivyotekelezwa.

## 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti Data katika utafiti huu zilikusanywa kwa usomaji wa maktaba na uchanganuzi makinifu wa matini. Kanda za nyiso za Wabukusu zilisikilizwa na kunakiliwa kwa maandishi. Usampulishaji wa kimakusudi ulifanywa katika uteuzi wa nyiso zilizohusu sifa za umahuluti wa kiutamaduni. Data zilichanganuliwa kithamano. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa mwa njia ya maelezo.

## 4. Matokeo ya Utafiti

Utafiti ulibainisha kwamba nyiso za Wabukuzsu zinadhihirisha sifa ya kuingiliana na kuhusisha utamaduni mwingine kwa njia ya matumizi ya lugha kwa vigezo mbalimbali ifuatavyo:

### 4.1. Ujumuilugha (heteroglosia)

Heteroglosia ni istilahi iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Kirusi anayefahamika kama Mikhail Bakhtin. Istilahi hiyo ilitokana na neno la Kirusi raznorechie alilolitolea fasili mbalimbali. Bakhtin (1981) alipambanua isilahi hii kuwili: katika mtazamo wa kiisimu na wa kifasihi. Mtazamo uliotumiwa katika matini hii ni ule wa kiisimu; kuwa ni hali ya matumizi ya zaidi ya lugha moja katika kauli.

O'grady na wenzake (1996) wanaeleza kuwa hakuna lugha yoyote ya kiasili iliyo "safi" au isiyoweza kuathiriwa na tamaduni na lugha nyingine zinazotagusana nayo. Hii ina maana kuwa katika mitagusano ya lugha, hutokea athari ambapo mifumo ya lugha huingiliana. Hili ni jambo lisiloweza kuepukika katika jamii zenye ujumuilugha. Iribemwangi (2011) na Simiyu (2011) wanaeleza kuwa ujumuilugha na hali ya mtu au jamii kutumia zaidi ya lugha mbili katika mawasiliano. Kibukusu ni lugha inayopatikana magharibi mwa taifa la Kenya. Lugha hii imetagusana na lugha nyingine nyingi katika Jumuia ya Afrika Mashariki na zaidi. Katika uchunguzi huu ilibainika kuwa nyiso za Wabukusu zinadhihirisha mitagusano ya lugha kwa njia ya kujumuisha zaidi ya lugha moja katika wimbo. Kwa mfano katika dondoo la 1 kutoka wimbo Shika polepole;

> Ndile polepole mai ese omukhasi wa bene busa
> Khamundile kalaa wandayase ndi omukhasi wa bene
> Ewewe mai esese ndi omusecha wa bene ano
> Kane okhole orio unjonakile enju
> Ndile polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi
> Nishike polepole mimi ni bwana ya wenyewe
> Nishike polepole maana ese ni bwana ya wenyewe
> Nishike polepole ujue mimi mchungaji
> Endile polepole omanye oli esese ng'ali omwilwachi
> wengine wanapiga solo wakisema baiskeli jifunze ya boma kwanza.
> Kamukuywa muli bakhasi ba bene
> Mukitali muli bakhasi ba bene
> Chunga machoinne, chunga we kepu
> Noli Father chunga bakhasi ba bene…
> *Beti za (1), (3) na (4)*

Katika dondoo hili, matumizi ya lugha yanabainisha hali zifuatazo:

i. Sehemu kubwa ya wimbo imo katika lugha ya Kibukusu

*Ndile polepole mai ese omukhasi wa bene busa* [Nishike polepole, mimi ni mke wa wenyewe]

*Khamundile kalaa wandayase ndi omukhasi wa bene* [...poleploe ndugu yangu, mimi ni mke wa wenyewe]

*Ewewe mai esese ndi omusecha wa bene ano* [Wewe mama, mimi ni muwe wa wenyewe hapa]

Maelezo haya yanaonesha mgogoro uliopo kati ya waume na wake, ambao wana ndoa zao, ila wanapitia majaribio ya mahaba nje ya ndoa. Hivyo wimbo unawahamasisha wahusika kuheshimu mipaka katika mahusiano yao, wahusiane kwa kuwajibika.

ii. Kuna matumizi ya kauli za lugha ya Kiswahili zilizokamilika pasipo kuchanganya na msimbo mwingine, mifano:

*Nishike polepole ujue mimi mchungaji*

**Nishike polepole mimi ni bwana ya wenyewe*

iii. Kuna matumizi ya kuchanganya misimbo ya Kiswahili, Kiingereza na Lubukusu

*Ndile polepole pastor* [Nishike polepole mhubiri].

**Ndile polepole mwenye ako na* jacket [Nishike polepole aliyevalia jaketi]

**Noli father chunga-* [ikiwa wewe ni kasisi, chunga].

iv. Kubadilisha msimbo kutoka Lubukusu hadi Kiswahili:

*Ndile polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi ×2* [Nishike polepole mwalimu...]

Wimbo huu umedhihirisha umahuluti kwa njia ya kushirikisha Kiswahili, Kiingereza na Kibukusu pamoja. Ingawa lugha ya Kibukusu ina msamiati ambao mwimbaji alikuwa na uhuru wa kuuteua na kuutumia, aliteua msamiati wa Kiswahili na Kingereza kimaksudi. Maneno haya yanawasilisha ujumbe alionuia kuwasilisha kwa uzito zaidi, kama wanavyochukulia wasomi (Myers-Scotton, 1993; Auer, 1998) ambao huchanganua uchanganyaji wa msimbo na ubadilishaji msimbo kama zana za kipragmatiki za msisitizo wa hoja. Ikumbukwe kwamba uchanganyaji wa misimbo na ubadilishaji misimbo sio tu matukio ya kiisimu bali ni matendo ya uhuru wa kitamaduni. Huwawezesha wazungumzaji kuabiri utambulisho wa baada ya ukoloni, kuunda mshikamano katika makundi tofauti, na kutoa upinzani kwa utawala wa lugha moja, hivyo, kushadidia maaelezo ya Bhabha (1994) kuwa umahuluti ni "nafasi mbadala yenye uhuru ya kujieleza." Barani Afrika, desturi hizi hubadilisha urithi wa kikoloni kuwa zana madhubuti za kujieleza, na kuthibitisha mtazamo wa Manessy (1995) wa umahuluti kama uthibitisho wa ubunifu wa lugha na uthabiti. Aidha, mifano katika dondoo la 2 kutoka wimbo Mulongo inadhihirisha ujumuilugha;

Ichunga mai ×2 Ichunga papa ×2 Ichunga senge ×2
Kang'ali kho mwichunge ×2 Kang'ali mbo mwichunge yaya×2
Khina kamabeka - khina mabeka kamabeka khwama engo
Khwesa ndombolo -khwesa ndombolo endombolo khwama engo
Eeh tila - tilaa, tila khumadamu
Eeh kosia - kosia, kosia khumadamu
Eeh tila, eeh tila mai - tila khumadamu
Eeh kosia, kosia mai - kosia khumadamu
*Beti za (2) na (3)*

Sehemu kubwa ya wimbo ni ya Kibukusu lakini pia kuna matumizi ya Kiingereza kwa mfano:

i. Tila khumadamu [mshike *madamu*]

Neno {*khumadam*} kimofolojia limeundwa kwa kuambisha kiambishi awali cha Kibukusu kwa mzizi wa Kingereza, yaani: {*khu*} + {*madam*} + {*u*}(kiambishi tamati {*u*} cha utaifishaji) ili kuunda neno {*khumadamu*}. Kwa mujibu wa Kihore, Kihore na wenzake (2012), uambishaji ni utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi. Mfano huu unaonesha uwezo wa lugha ya Kibukusu kutumia viungo vyake vya kiisimu na kuungana na kipashio cha lugha tofauti ili kuunda kipashio kinachodhihirisha mseto wa kiisimu.

ii. Pia kuna matumizi ya neno la lahaja ya Kilingala kwa mfano:

Khwesa *ndombolo* [cheza densi ya ndombolo]

Wimbo huu unadhihirisha matumizi ya mseto wa Kiingereza, Kilingala na Kibukusu. Uwezo wa kuambisha viambishi vya lugha moja na mzizi wa lugha tofauti, na matumizi ya maneno ya lahaja tofauti ni mfano wa jinsi dhana ya ubunifu wa lugha inavyojitokeza katika umahuluti wa kiisimu (Manessy, 1995).

Aidha, dondoo la 3, kutoka wimbo Sponsor ladhihirisha mitagusano ya lugha nyingi.

Sponsor bano batimilanga mumatoka kamanyifu
Sponsor bano bombakha chipuloti khusialo
Sponsor bano nibo bakula chindeke khusialo
Sponsor bano balala bainjinia nibo
Sponsor bano babandi wanasiasa
Ewe siponsor ndila...
Mwonaka kamasomo,
Kila kitu ni mosmos, iko kitu mbele.
*Beti za (4), (5) na (6)*

Sehemu kubwa ina matumizi ya lugha ya Kibukusu lakini ndani mwake, kuna matumizi ya lugha mbalimbali kama vile:

i. Kiswahili: *babandi wanasiasa* [wengine ni wanasiasa]
ii. Kijaluo: kila kitu ni *mosmos* [Kila kitu kifanyike polepole/taratibu]
iii. Kiingereza: *Sponsor* [Mfadhili]

Aidha, kuna dhihirisho la uambishaji wa viambishi vya Lubukusu katika maneno yenye asili ya Kiswahili. Mifano ni kama vile:

Vipashio {mu} + {ma} + {toka} vinaunda {mumatoka} [kwa motokaa/magari]

Vipashio {chi} + {ndeke} vinaunda {chindeke} [∅ndege}

Mifano kama hii imetolewa na Gathiora (2018), akishughulikia lugha ya "Sheng". Hebu tazama:

*Fala msee aliniscam* [Fala aliniibia]

Neno *aliniscam* ni mseto wa viambishi vya Kiswahili {a}+{li}+{ni} na mzizi wa Kiingereza {*scam*}. Aidha Gathiora ametoa mfano wa pili ambao ni, "Alinisave kwa hio gava". Mifano hii inaonesha matumizi ya miundo mahuluti katika kitenzi na nonimo.

Kwa ujumla umahuluti wa kiisimu katika nyiso umebainika kupitia ujumuilugha ambapo kando na matumizi ya Kibukusu, kuna matumizi ya Kiingereza, Kiswahili, Kilingala na Kiluo. Hili ni dhihirisho kuwa lugha zinapodumu katika hali ya kutagusana, huishi zikiathiriana. Athari hizi hujitokeza katika maumbo ya kileksia ama kisintaksia. Sehemu ifuatayo inajadili miundo ya kiisimu iliyobainishwa katika nyiso.

## 4.2. Miundo ya umahuluti wa Kiisimu katika Nyiso za Wabukusu

Dhana Miundo mbalimbali ya vipashio vya ujenzi wa lugha vinavyodhihirisha umahuluti wa kiisimu kama ulivyojitokeza katika nyiso imebainishwa ifuatavyo.

## 4.3. Miundo ya manenoi.

### *4.3.1. Ukopaji*

anabainisha Dahana ya ukopaji inarejelea tendo la kuchukua istilahi au msamiati wa lugha moja na kuutumia kama msamiati katika lugha nyingine (Kiango, 2002), akinukuliwa na Kihore na wenzake (2012). Hii ni mbinu mojawapo ambayo imetumika sana kunda msamiati na istilahi katika lugha nyingi duniani ili kukidhi haja ya mawasiliano (Matinde, 2012). Aidha, ameeleza kwamba ukopaji katika lugha unafanyika kwa kutumia mbinu za utohozi, ukopaji kwa tafsiri na ukopaji sisisi. Katika nyiso za Wabukusu tulizorejelea, ukopaji kupitia utohozi na ukopaji kwa tafsiri ni mbinu kuu zinazojitokeza.

### *4.3.2. Utohozi*

Utohozi ni mbinu ya uundaji wa maneno inayoruhusu lugha lengwa kubadili umbo na matamshi ya neno lililokopwa ili lioane na tahajia na mofolojia ya lugha pokezi (Obuchi & Sangili, 2016). Jambo hili huwezesha neno husika kuendelezwa na kutamkwa kwa mujibu wa kanuni za lugha lengwa. Hali hii imedhihirika kupitia mifano katika dondoo la 4, wimbo Nishike polepole:

> Ndile polepole ndile polepole *daktari*, shika polepole ese omukhasi wa bene
> Ndile polepole ndile polepole *dijei*, shika polepole ese omukhasi wa bene
> wengine wanapiga solo wakisema *baiskeli* jifunze ya boma kwanza
> *Beti za (2) na (4)*

Maumbo ya maneno yaliyokopwa kwa kutoholewa yamejitokeza katika wimbo kama ifuatavyo:

> Nishike polepole *dijei*; [utohozi wa Kimombo DJ-disco jockey]
> ndile polepole *daktari*, [utohozi wa neno la Kingereza-doctor]
> wanapiga solo wakisema *baiskeli* [utohozi wa neno la Kingereza bicycle]

Katika dondoo la 5, wimbo Sponsor mwimbaji anasema;

> Ewe siponsa, we wasio
> Yakhaba basomi, we wasio
> Sponsor bano bombakha chipuloti khusialo
> Sponsor bano balala bainjinia nibo
> Bawechanga babana chilifti,
> Bali khumushahara
> Sponsor bano nibo bakula chindeke khusialo
> *Beti za (1), (3), (4) na (6)*

Dondoo hili kutoka wimbo Sponsor limedhihirisha mifano kadhaa ya utohozi. Baadhi ya maneno yaliyoingizwa katika mfumo wa Kibukusu yametoholewa kutoka kwa yale ya Kingereza na mengine kutoka kwa maneno ya Kiswahili, ambayo nayo ni matokeo ya utohozi kutoka kwa Kiingereza. Kwa mfano:

> Enywe *siponsa* [Ninyi *sponsa*] lililotoholewa kutoka kwa Kingereza "sponsor"]
> Bawechanga babana *chilifti* [wanaowapa watoto *lifti* la Kiswahili, lililotoholewa kutoka kwa neno la Kingereza yaani "lifts"
> Bali *khumushahara* [wana mishahara] Kutokana na utohozi wa neno la Kiswahili "mshahara"
> *Sponsor* bano nibo bakula chindeke khusialo [utohozi wa neno ndege]
> bano balala bainjinia [wengine ni *mainjinia*] [kutokana na utohozi wa neno la Kingereza, *engineer*].

Mifano katika nyiso hizi inadhihirisha uingizwaji wa maneno yanayoashiria dhana za kigeni zilizoingizwa katika utamaduni wa Wabukusu kama vile lifti, mshahara, baiskeli, wasomi miongoni mwa nyingine. Ukopaji huu hautokei tu. Kuna sababu za kutokea kwake. Matinde (2012) ametaja kwamba, ukopaji unatokana na sababu kadhaa zikiwemo; kuzuka kwa dhana mpya katika jamii, mtagusano wa tamaduni mbili kwa muda mrefu. Sababu nyingine ni kasumba ya wazungumzaji wa lugha ya kukopa, pamoja na utabaka-jamii mbili ambazo zinatofautiana katika nguvu za kisiasa na kiuchumi.

### *4.3.3. Ukopaji kwa kutafsiri*

Ukopaji kwa tafsiri ni mbinu inayohusisha maneno au vifungu katika lugha chanzi kufasiriwa katika lugha pokezi (Matinde, 2012). Kuna msamiati ambao umekopwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza na kutumiwa vivyo hivyo ingawa visawe vyake katika lugha pokezi vipo. Msamiati mwingine umetafsiriwa katika lugha pokezi. Tazama mifano kutoka katika dondoo la 6, wimbo Nishike polepole.

> Ndile polepole ndile polepole *pastor* - shika polepole ese omukhasi wa bene
> Ndile polepole ndile polepole mwenye ako na *jacket* - shika polepole ese omukhasi wa bene
> Nishike polepole ujue mimi *mchungaji*
> Noli *Father* chunga bakhasi ba bene
> *Beti za (1), (2), (3) na (4)*

Neno pastor limetumika katika wimbo mara mbili. Kwanza, limetokea katika umbo asilia la lugha chanzi yaani, pastor, bila kutafsiriwa Pili, limetokea kama tafsiri katika lugha ya Kiswahili, mchungaji Aidha, kuna matumizi ya maneno ya Kingereza, father na jacket. Maneno haya yana visawe na kama yangefasiriwa katika lugha ya Kiswahili, Father lingekuwa kasisi, na jacket lingekuwa jaketi. Hali hii ya matumizi inaonesha namna ambavyo mwimbaji anadhihirisha ukopaji kama njia ya kuonesha ukwasi wake wa msamiati wa lugha ya Kingereza (TUKI, 2005). Tafsiri ni mchakato unaoleta pamoja tamaduni mbili kupitia lugha za matini chasili na matini pokezi. Hivyo basi tasnia ya tafsiri na mawasiliano kati ya tamaduni anuwai inachangia kuleta umahuluti wa kiisimu. Kama anavyosema Klinger (2015), umahuluti wa kiisimu ni sifa ya kawaida ya matini ambazo hutafsiriwa katika mipaka ya lugha na utamaduni—iwe tafsiri ya kawaida kati ya lugha kutoka matini chanzi (MC) hadi matini lengwa (ML) au aina nyinginezo za tafsiri ambazo hazina MC inayoonekana kama vile maandishi ya wahamiaji, au ya baada ukoloni.

### 4.4. Miundo ya Kisintaksia

wanauhakiki Umahuluti katika nyiso pia umejidhihirisha katika kiwango cha kisintaksia. Hii ni mifano inayojitokeza kupitia miundo ya virai, vishazi au sentensi kwa njia zifuatazo:

#### *4.4.1. Ubadilishaji na Kuchanganya Msimbo*

Ingawa dhana za ubadilishaji msimbo na kuchanganya msimbo zimefasiliwa na wataalamu wengi, bado kuna mjadala kuzihusu. Uchanganyaji msimbo hapo awali ulielezwa kuwa ni kutumia maneno na vishazi kutoka lugha moja badala ya yale ya lugha nyingine ndani ya sentensi moja- yaani, ambapo kubadili lugha hutokea ndani ya sentensi moja (Sridhar & Sridhar, 1980). Kwa upande mwingine, ubadilishaji msimbo umeelezewa kuwa ni kubadili kati ya lugha kulingana na mabadiliko katika hali ya usemi, ambapo mada au wahusika wa mazungumzo hubadilika (Altarriba & Santiago-Rivera, 1994). Hii ina maana kwamba ubadilishaji msimbo hautokei ndani ya sentensi, ila uchanganyaji msimbo ni wa ndani ya sentensi na hautegemei mabadiliko ya hali katika mazungumzo (Sridhar & Sridhar, 1980).

Kwa kuwa lengo la makala hii siyo kujadili tofauti kati ya dhana hizi mbili, bali kuonesha udhihirikaji wake kama uhalisia wa matumizi ya lugha katika muktadha wa umahuluti, makala hii inarejelea ubadilishaji kama tukio, iwe ndani ya mada, aya, au sentensi. Kwa kufanya hivyo, tunaegemea maoni ya Cromdal (2000) anapoeleza kuwa ubadilishaji msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika sentensi moja au mfuatano wa sentensi nyingi kati ya watu wawili au zaidi. Maoni ya Odeo & Maina (2008), kuwa ubadilishaji msimbo ni hali ambapo mzungumzaji anasema katika lugha moja kisha baada ya muda akaongea kwa lugha ya pili na kuweza kuongea kwa muda yanaelekea kusawiana na yale ya Cromdal (2000). Ubadilishaji au uchanganyaji msimbo hutokana na uwezo wa mzungumzaji kufahamu zaidi ya lugha moja. Licha ya maelezo tofauti, inabainika kuwa ubadilishaji msimbo hutokea panapokuwa na matumizi ya zaidi ya lugha moja katika mazungumzo, kama ilivyojitokeza katika dondoo la 7, wimbo Nishike Polepole.

> Ewewe mai esese ndi omusecha wa bene ano
> Kane okhole orio unjonakile enju
> Ndile polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi ×2
> *Ubeti (3)*

Ndile *polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi* [Nishike polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi]. Kishazi [*polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi*] msimbo wa Kiswahili ambao. Mwimbaji alianza kwa kauli ya Kibukusu [*ndile*], kisha akabadilisha kabisa na kukamilisha katika Kiswahili. Aidha, *Shika polepole ese omukhasi wa bene* [niguze polepole mimi ni mke wa mwenyewe]. Hapa alianza kwa Kiswahili kisha akaendeleza kwa Kibukusu.

#### *4.4.2. Kuchanganya Msimbo*

Muysken (2000) anaeleza kuwa 36ap ana mazingira yote ambapo kipengele kimoja cha kileksia na sehemu ya sarufi kutoka lugha mbili tofauti huchanganywa au kutokea kwa 36ap an katika sentensi moja. Aidha wasemavyo Iribemwangi (2011) na Simiyu (2011), ni hali ya mtumiaji lugha kuzungumza katika lugha moja kisha 36ap ana pale anatoka katika lugha hiyo na kuingilia lugha ya pili au ya tatu kwa muda mfupi na kisha kurejelea lugha ya awali. Hapa kuna mabadiliko ya 36ap ana pale katika umbo neno katika utungo na hali hii hutokea katika muktadha wa uwililugha au wingilugha. Katika dondoo la 8 wimbo Nishike polepole kuna kauli zifuatazo:

> *Ndile* polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi ×2
> Nishike polepole maana ese ni bwana ya wenyewe
> Ndile polepole ndile polepole *mwenye* kofia
> *Beti za (2) na (3)*

Katika mshororo Nishike polepole maana ese ni bwana ya wenyewe; mwimbaji ameanza kwa msimbo wa Kiswahili kisha Kibukusu [ese] halafu anakamilisha kwa msimbo wa Kiswahili. Pia, katika Ndile polepole ndile polepole mwenye kofia; amechanganya msimbo kwa kuanza na wa Kibukusu kisha Kiswahili, halafu Kibukusu kisha Kiswahili tena.

### 4.5. Kiwango cha Maana

Nyiso zimedhihirisha ukopaji wa msamiati unaoleta maana fulani. Hii imefaulishwa katika baadhi ya nyiso kupitia kwa misemo.

#### *4.5.1. Tafsiri*

Tafsiri imefasiliwa na Simiyu (2012) kuwa ni uhawilishaji wa ujumbe kwa njia ya maandishi pamoja na uamilifu wake kutoka lugha chasili hadi lugha lengwa kwa mujibu wa isimu, muktadha na utamaduni wa lugha zote. Lugha inayotumiwa katika nyiso imebainisha hali ya kuwasilisha ujumbe ambapo lugha moja inaangaza nyingine kwa kutumiwa pamoja katika matini moja. Haya yamedhihirika katika utanzu kupitia muundo wa neno, sintaksia na kiwango cha semantiki.

#### *4.5.2. Tafsiri Sisisi*

Matumizi ta tafsiri sisisi, ambayo ni ufasiri wa maana za kimsingi za maneno yakiwa pwekepweke kwa kuzingatia kanuni za kisarufi za lugha pokezi (Simiyu, 2012). Kuna tafsiri ya neno kwa neno kama vile katika dondoo la 9, wimbo Nishike polepole:

> Shika polepole ese omukhasi wa bene
> Shika polepole shika polepole
> Ndile polepole ndile polepole
> Khamundile kalaa wandayase ndi omukhasi wa bene
> *Beti za (1), (2) na (3)*

Katika mfano huu, tafsiri sisisi ya Kibukusu ya ndile kalaa (matini chanzi) ni shika polepole (matini pokezi).

### 4.6. Uegemezaji wa utamaduni wenye nguvu katika nyiso

Utamaduni wenye na nguvu ni dhana inayorejelea kundi lililowezeshwa kijamii na kisiasa ambalo lugha yake, kanuni, na desturi zimewekwa kama kigezo au chaguo la msingi katika jamii, huku likitenga mifumo mingine ya kiisimu au kitamaduni (Bhabha, 1994). Katika umahuluti wa lugha, dhan hiyo inawakilisha nguvu za kimamlaka ambazo sifa za umahuluti zinalenga kupinga, kukiuka au kupindua. Utamaduni

ulio na nguvu hushurutisha matumizi ya lugha yake kwa mfano, Kiingereza au Kifaransa katika muktadha wa baada ukoloni, kama msimbo "bora", na kuacha lugha za kiasili zikitazamwa kuwa za hadhi duni. Umahuluti wa kiisimu unajitokeza wakati ambapo wazungumzaji waliotengwa wanachanganya misimbo ya lugha kuu, zenye nguvu kubwa na zile ndogo kuunda "nafasi mbadala" ya mawasiliano ya kitamaduni. Mfano wa hali hii inavyojitokeza nchini Kenya ni pale wasomi wanapotumia Kiingereza katika maeneo rasmi, dhidi ya matumizi ya Sheng katika miktadha isiyo rasmi na miktadha ya kijamii kama upinzani wa matumizi ya Kingereza (Muriira, 2016).

Ingawa nyiso za za Wabukusu pia zilidhihirisha umahuluti, haukuwa kwa njia ya kupinga ama kuasi, bali kwa njia ya kupokea na kuegemeza utamaduni wenye nguvu kwa matumizi ya msamiati wa lugha ili kutekeleza majukumu yake katika jamii. Nyiso zilisheheni maudhui ya miviga na matambiko mbalimbali yanayohusu tohara. Hata hivyo, kuna maudhui mbalimbali yaliyoshirikishwa kutokana na matukio yaliyopewa kipaumbele katika jamii katika taasisi mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katika wimbo Shika polepole, maudhui ya dini ya Kikristo yamejitokeza katika mifano ifuatayo ilivyodhihirika katika dondoo la 6, *(Beti za (1), (2), (3) na (4)*:

> *Ndile polepole ndile polepole* ***pastor*** [nishike polepole niguze polepole mhubiri]. Mwimbaji anamsihi mhubiri amshike polepole.
> *Noli* ***Father*** *chunga bakhasi ba bene*. [Ukiwa kasisi, tahadhari na wake wa wenyewe] hapa, mwimbaji anawashauri na kuwasihi walio makasisi watahadhari, wasiwe wepesi wa kuwanyemelea wake wa wenyewe.
> *Endile polepole omanye oli esese ng'ali* ***omwilwachi*** [nishike polepole ujue kuwa kweli mimi ni mhubiri]. *Nishike polepole ujue mimi* ***mchungaji***.

Kuchopekwa huku kwa msamiati wa kidini kunaonesha kuwa jamii imekubali uwepo wa dini ya Kikristo sambamba na utamaduni wa jamii. Kauli hii imetiliwa nguvu na utafiti wa Wagner (1949) katika Namulunda (2011) aliposema kwamba dini ya Kikristo imeathiri pakubwa utamaduni wa Wabukusu. Viongozi wa jamii wapo katika koo mbalimbali lakini jamii inatambua uwepo na umuhimu wa viongozi wa kidini. Nafasi ya dini imetambuliwa katika kuadilisha jamii na hili limedhihirishwa kwa wito unaotolewa kwa viongozi wa kidini kudumisha maadili na kuadilisha jamii. Wamehusishwa katika nyiso katika ujumlifu wa uhalisia wa maingiliano ya tamaduni na dini katika jamii. Hivyo wanatahadharishwa katika kuhusika katika mambo ya kunyumbua jamii, hasa kuvunja ndoa za watu. Mwimbaji wa wimbo huu amemtaja kiongozi huyu wa dini katika ndimi tatu (Kiingereza-pastor, Kiswahili-mchungaji na Kibukusu-omwilwachi). Amefanya hivi kwa kurejelea majina yanayotumiwa kwa viongozi wa dini katika madhehebu tofauti, kama njia ya kutoa msisitizo wa ujumbe kwa anaye elekezewa.

Kuna mtazamo kubalifu katika dini kuwa viongozi wa dini ni walinzi wa kondoo. Jambo hili limejitokeza katika msamiati wachungaji. Yesu akiongea na mfuasi wake aitwaye Petero katika Biblia katika kitabu cha Yohana mlango wa tano mstari wa kumi na saba anamwambia: lisha kondoo wangu. Hivyo kiongozi wa kidini amerejelewa kama mchungaji wa kondoo kando na kurejelewa tena kama omwilwachi (Kibukusu) na pastor pamoja na Father kwa Kiingereza katika wimbo huo huo.

Utamaduni wa densi za kigeni pia umeeegemezwa katika nyiso za Kibukusu. Jamii ya Wabukusu kama zilivyo jamii nyingine za Kiluhya ni maarafu katika densi za mabega. Densi hiyo imehusishwa katika nyiso ifuatavyo. Katika dondoo la 2, wimbo Mulongo mwimbaji anasema;

Sena mabeka kamabeka khwamaengo [tingiza mabega mabega mtindo kutoka nyumbani]. Hata hivyo kuna densi maarafu yenye asili ya Congo ijulikanayo kama ndombolo ambayo imeegemezwa kama mwondoko uliopo katika jamii. Mwimbaji anasema, Khwesa ndombolo endombolo khwamengo [cheza densi ya ndombolo mtindo wa nyumbani].

Densi ya ndombolo imeegemezwa pasipo mikwaruzano ya tamaduni hizi mbili. Huu ni ufikirio mpya katika wimbo unaoonesha utangamano na ujumulifu wa kiutamaduni.

Aidha katika maudhui, suala ibuka la gonjwa sugu la UKIMWI limepata nafasi katika nyiso. Suala la UKIMWI limekuwa diskosi kwa muda tangu lizuke na upenyezi wake umefikia nyiso za Wabukusu kwa lengo la kutahadharisha jamii. Dondoo 11 katika wimbo Mlongo linabainisha ushauri huu msanii anaposema;

> Kang'ali ichunga mai – ichunga bulwale buli simbi bwolile
> Kang'ali enywe ilinda mai- ilinda bulwale buli simbi bwolile
> Sena kamabeka- sena kamabeka kamabeka kwama engo
> Ubeti (1)

Katika dondoo hili, msanii anasema, Kang'ali ichunga mai [hakika tahadhari mama]. Ilinda bulwale buli simbi bwolile [Jilinde ugonjwa uko karibu na umefika]. Mwimbaji anaishauri jamii kuwa kuna tishio la ugonjwa hatari.

Aidha, kuna suala ibuka la Sponsor ambapo msanii anasema, esindu bali siponsa [kitu eti sponsa]. Hawa ni wanaume na wanawake wafadhili wanaojitolea kuwasaidia watu kumbe wana lengo fiche linaloathiri pakubwa wanaosaidiwa. Mwimbaji anakiri katika wimbo kuwa hili ni jambo jipya katika jamii ambalo linaleta aibu na hasara

## 5. Hitimisho

Makala hii imebainisha kuwa nyiso zinadhihirisha umahuluti wa kiisimu. Makala imeonesha kwamba kwa kuwa lugha inabadilika kila wakati, watu huboresha lugha zao kupitia kujumuisha vipengele fulani vya lugha kutoka kwa tamaduni nyingine. Kwa kufanya hivyo,

maneno mapya yanaundwa na kuingizwa ili kuendana na sehemu ya mawasiliano ya kijamii ya lugha pokezi. Aidha, imebainika kwamba, licha ya jamii ya Wabukusu kusharabu sifa za kiisimu kutoka kwa lugha nyingine, mivigha ya tohara ya Bukusu imehifadhiwa. Hii inamaanisha kuwa tamaduni zinaweza kuishi pamoja na hivyo kuunda maelewano ya kitamaduni.

## Marejeleo

Ackermann, A. (2012). Cultural Hybridity: Betweeen Metaphor and Empiricism. In P. Stockhammer, Conceptualizing Cultural Hybridization: A Transdisciplinary Approach. New York: Springer Publishers.

Altarriba, J., & Santiago-Rivera, A.L. (1994). Current perspectives on using linguistic and cultural factors in counseling the Hispanic client. Professional Psychology: Research and Practice, 25, 388-397.

Auer, P. (Ed.). (1998). Code-Switching in Conversation: Language, Interaction and Identity. London: Routledge.

Bakhtin, M. (1981). The Dialogic Imagination: Four Essays. Edited by Michael Holquist. Translated by Caryl Emerson and Michael Holquist. Austin: University of Texas Press.

Bhabha, H. K. (1994). The Location of Culture. London: Routledge.

Bhabha,H.K.(1997).Of mimicry and Man:The ambivalence of colonial discourse.In F.Cooper&A.L.Stoler(Eds), Tensionsof Empire:Colonial Cultures in a Bourgeois World(pp.152-160).University of Carlifornia Press.

Cromdol, J. (2000). Code Switching for all Practical Purposes, Bilingual Organization Of Children's Play. New York: St Mattin's Press Inc.

Demska, O. (2019). Hybridity and the linguistic landscape. Cognitive Studies/ Études cognitives, 2019(19). https://doi.org/10.11649/cs.2007

Githiora, C. (2018). Sheng: Rise of a Kenyan Swahili Vernacular. Woodbridge: James Currey.

Habwe, J. & Zaja, J. (2019). Kamusi ya Isimu na Fasihi. Nairobi: Printing Services Limited.

Iribemwangi, P. & Mukhwana, A. (2011). Isimujamii. Nairobi: Printpak Publishers.

Kihore, Y. M,. Massamba, D. P. B. & Msanjila, Y. P. (2012). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Klinger, S. (2002) (Ed). Translation and Linguistic Hybridity: Constructing World View. New York: Routeledge.

Koech, J. C. (2024). Umahuluti wa Utamaduni katika Nyimbo za Harusi Miongoni mwa Wanandi. East African Journal of Swahili Studies, 7(2), 214-241. https://doi.org/10.37284/jammk.7.2.2514

Manessy, G. (1995). Créoles, pidgins, variétés véhiculaires: Procès et genèse. Paris: CNRS Éditions.

Matei, A. (2011). Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili. Nairobi: Oxford University Press.

Matinde, R. (2012). Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia. Tanzania: Serengeti Educational Publishers.

Matinde, S. (2012). Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia kwa Sekondari, Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu. Mwanza,: Serengeti Educational Publishers.

Muriira, M. P. (2016). A Complex Linguistic Code in Kenyan Linguistic Scene: A Case Study For Sheng. Master of Arts Thesis. University of Nairobi. (Unpublished).

Muysken, P. (2000). Bilingual Speech. A Typology of Code Switching. Cambridge: Cambridge University Press.

Myers-Scotton, Carol. 1993. Social Motivations for Codeswitching: Evidence from Africa. Oxford: Clarendon Press.

Namulunda, F. (2011). The Bukusus of Kenya Folktales, Culture and Social Identities. North Carolina: Carolona Academic Press.

Obuchi, S. M. & Sangili, N. K. N. (2016). Taaluma ya Maana: Semantiki na Pragmatiki. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Odeo, I & Maina, G. (2008). Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari. Nairobi: Oxford University Press.

O'grady, W; Dobrovolsky, M; Katamba, F. (1996). Contemporary Linguistics: An Introduction. United Kingdom: Copp Clark Pitman Limited.

Shatry,A.(1996). Tamaduni na Fasihi za Kienyeji kwa Lugha za Kigeni.APP 47. Kur. 97-107

Simiyu, C. & Mukhwana, A. (2016). The Images of Men and Women: A Lexical- Pragmatic Approach to Lexical Choices of Selected Bukusu Circumcision Songs. International Journal of Education and Research, Vol.4 No. 9.

Simiyu, F. W. (2011). Kitovu cha Fasihi Simulizi Kwa Shule, Vyuo na Ndaki. Tanzania: Serengeti Educational Publishers.

Simiyu, F. W. (2012). Misingi ya Ukalimani na Taf siri Kwa Shule, Vyuo na Ndaki. Tanzania: Serengeti Educational Publishers.

Simiyu, F. W. (2015). Mwingilianotanzu Katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa . Chuo Kikuu cha Kenyatta: Tasnifu ya Uzamifu.

Sridhar, S.N., & Sridhar, K.K. (1980). The syntax and psycholinguistics of bilingual code mixing. Canadian Journal of Psychology, 34, 407-416.

TUKI (2005). Sarufi Maumbo ya Maneno na Vinyambulisho. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Wamitila, K.W. (2004). Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi. Nairobi: English Press

Wanyama, M. (2005). Form and Content of African Music: A Case Study of Bukusu Circumcision Music. University of Pretoria.

## KIAMBATISHO A: SHIKA POLE POLE

1. Shika polepole ese omukhasi wa bene - shika polepole ese omukhasi wa bene
Shika polepole shika polepole -- shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole pastor - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole mwalimu - shika polepole ese omukhasi wa bene

2. Ndile polepole ndile polepole daktari - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole dijei - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole kijana - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole macho inne - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole mwenye ako na jacket - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole ndile polepole mwenye kofia - shika polepole ese omukhasi wa bene
Ndile polepole mai ese omukhasi wa bene busa

3. Khamundile kalaa wandayase ndi omukhasi wa bene
Ewewe mai esese ndi omusecha wa bene ano
Kane okhole orio unjonakile enju
Ndile polepole mwalimu mimi bado mwanafunzi ×2
Nishike polepole mimi ni bwana ya wenyewe
Nishike polepole maana ese ni bwana ya wenyewe
Nishike polepole ujue mimi mchungaji
4. Endile polepole omanye oli esese ng'ali omwilwachi
( wengine wanapiga solo wakisema baiskeli jifunze ya boma kwanza..)
Kamukuywa muli bakhasi ba bene
Mukitali muli bakhasi ba bene
Chunga machoinne, chunga we kepu
Noli Father chunga bakhasi ba bene…

## KIAMBATISHO B: MULONGO

1. KIITIKIO
Kang'ali ichunga mai - ichunga bulwale buli simbi bwolile
Kang'ali enywe ilinda mai- ilinda bulwale buli simbi bwolile
Sena kamabeka- sena kamabeka kamabeka kwama engo

2. Ichunga mai ×2 Ichunga papa ×2 Ichunga senge ×2
Kang'ali kho mwichunge ×2 Kang'ali mbo mwichunge yaya×2
Khina kamabeka - khina mabeka kamabeka khwama engo
Khwesa ndombolo -khwesa ndombolo endombolo khwama engo

3. Eeh tila - tilaa, tila khumadamu
Eeh kosia - kosia, kosia khumadamu
Eeh tila, eeh tila mai - tila khumadamu
Eeh kosia, kosia mai - kosia khumadamu
(Bwasiele muluma, kumubano kwaluma)

4. Mulongo - hahoo ×2
Wamwene weyama yaya - hahoo
Mwana wa papa oluma- hahoo ×2
Mwana wa mai oluma- hahoo ×2
Mwana wa khocha oluma -hahoo ×2
Mwana wa mai oluma - hahoo ×2
Lukembe lurafu yaya - hahoo ×2
Mubandu lwalula yaya - hahoo ×2
Balimbele khulaini, khane omwana akwa munda
Aah mai balimbele khulaini, khane omwana akwa munda Kiitikio

## KIAMBATISHO C : SPONSOR

1. Sponsor we sponsor - we wasio
Ewe sponsor- we wasio
Sponsor wamalile babana- we wasio
Ewe sponsor- we wasio
Sponsor wamalile basomi - we wasio

2. Yakhaba bamayi - we wasio
Muchikanisa- we wasio
Mubaa - we wasio
Muchiloching'i - we wasio
Yakhaba mulandi - we wasio
Yakhaba mwitoka - we wasio

3. Ewe siponsa - we wasio
Wamalile babana- we wasio
Yakhaba basomi- we wasio
Enywe enywe
Enywe siponsa
Mwamalile babana

4. Sindu bali siponsa, olwo lulumbe
Lekha mbabolelekho
Sponsor bano batimilanga mumatoka kamanyifu
Sponsor bano bombakha chipuloti khusialo
Sponsor bano nibo bakula chindeke khusialo
Sponsor bano balala bainjinia nibo
Sponsor bano babandi wanasiasa

5. Ewe siponsor ndila
Warerire lulumbe khusialo
Khamumbolele
Enywe siponsa
Mwakholile chisoni
Yakhaba omwana bali asoma, sponsor yuno

6. Mwonaka kamasomo,
Kila kitu ni mosmos, iko kitu mbele.
Iko nini Transnzoia
Bawechanga babana chilifti,
Bali khumushahara
KCA bechile baninisye bikioo bimali kecha…